# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

**19 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA TISA - TAREHE 19 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**626 MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kwa nini Pensheni hazibadiliki na kupanda kutokana na mfumuko wa bei.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**627 MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni maeneo gani ya kuweka mkazo ili Sekta nyingine zitekeleze na kuwa sehemu ya utekelezaji wa azma ya Ugatuzi wa Madaraka.

**WIZARA YA NISHATI:**

**628 MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itatatua tatizo la kukosa huduma ya umeme katika Vitongoji vya Jimbo la Tabora Mjini.

**629 MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, zipi sababu za kuwa na gharama tofauti ya kuingiza Umeme majumbani Kibaha Vijijini badala ya kuwa na bei moja ya Shilingi 27,000 tu.

**WIZARA YA UJENZI:**

**630 MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya mchepuko ya Mlima Nyoka kutoka Uyole hadi Songwe.

**631 MHESHIMIWA ASK. JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga mitaro ya maji kuanzia Tegeta hadi Basihaya ili kumaliza athari za mafuriko kila mwaka.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**632 MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litakuwa na Ofisi ya kuendesha shughuli zake katika Wilaya ya Nyasa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**633 MHESHIMIWA ZUENA ATHUMAN BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Skimu ya Umwagiliaji itajengwa katika Kata ya Arusha Chini Moshi Vijijini.

**634 MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini kilimo cha Mazao ya Alizeti na Chikichi kitaanza Mkoani Kagera kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais akiwa Bukoba Juni, 2022.

**WIZARA YA MAJI:**

**635 MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Maji Kata ya Uwemba – Njombe Mjini.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**19 JUNI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA